



## Maswali na Majibu

1. Maisha yetu yanabadilikaje baada ya ubatizo?  
*Tusiishi maisha ya kujipendeza sisi wenyewe lakini tumpendeze Mungu pamoja na Yesu.*
2. Mambo gani 4 yaliyo ya muhimu kwa maisha ya Mkristo?  
*Mafundisho ya mitume kuhusu Yesu, ushirika, kumega mkate na maombi.*
3. Mafundisho ya mitume ni nini?  
*Mafundisho ya mitume ni kuhusu Yesu. Iliandikwa kwa Agano Jipy.*
4. Tufanyeje ili tujifunze mafundisho ya Mungu? *Soma Biblia kila siku.*
5. Tunakuwa na ushirika na nani?  
*Mungu na Yesu pamoja na ndugu na dada katika Yesu.*
6. Mbona tusiende tuwe na ushirika na makanisa mengine?  
*Ushirika wa maana ni tuwe na Mungu, tunapaswa kushirikiana na wale walio na ukweli wa Mungu.*
7. Mwisho wa chakula cha mwisho na wanafunzi wake, Yesu alifanya nini?  
*Alivunja mkate na akamwaga divai kwa kikombe. Aliambia wanafunzi wake wawe wakifanya hivyo wakikumbuka vile alikufa kwa kuwaokoa kutoka dhambini.*
8. Inajalisha ni lini au ni wapi Wakristo wanakutana kumega mkate?  
*Hapana. Yesu atakuwa na wale wanaomega mkate kwa Imani ya kweli.*
9. Tunaweza kumega mkate na wale wasiobatizwa?  
*Hapana. Hawako kwa ushirika wa kweli na Mungu na Yesu.*
10. Tunapazwa kufanya nini tena ili tuwe karibu na Mungu?  
*Kuomba Mungu kila wakati.*

## Mistari ya kukariri

Matendo 2:42            Mathayo 18:20            1 Yohana 1:3

## Mazungumzo

Zungumza juu ya mambo 4 ya muhimu kwa maisha ya Mkristo. Eleza vile tunaweza kuweka haya mambo 4 kwa maisha ya kila siku.

## Kuandika

Andika juu ya ushirika wa Mkristo na nini inafanya iwe ya muhimu.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 43 Maisha ya Ukristo.

**SOMA** 1 Wakorintho 13; 2 Timotheo 3:14 – 17; Mathayo 18:20;  
Mathayo 5:3 – 10; & 43 – 48; 1 Yohana 1:3; Matendo 2:42

### SOMO

Ubatizo ni mwanzo wa maisha mapya katika Kristo kwa waumini. Mwanzo mpya huleta mabadiliko. Baada ya ubatizo tunaanza kuishi maisha ya kumpendeza Mungu na Yesu sio sisi wenyewe.

**Mafundisho ya Mitume**  
**Ushirika**  
**Kumega mkate**  
**Maombi**

Soma Matendo 2:41 – 42. Kuna mambo manne yaliyo ya maana kwa maisha mapya ya wanafunzi: Kumbuka Biblia imesema ‘walidumu’ (wenyewe walijitoa) kwa haya mambo manne. Hii inamaanisha waliendelea kufanya hivyo kila wakati na hawakuacha. Hawakuanza na mioto halafu baada ya majuma machache wakaacha. Haya mambo manne yalitendwa kila mara na yalikuwa ya maana katika maisha yao ya kila siku mpaka walipokufa. Ukibatizwa na kuanza maisha ya Ukristo ni hali ya kujitolea – ni ahadi ya vile utaishi kwa maisha yako yote.

### Mafundisho ya Mitume

Mafundisho ya Mitume ni mafundisho juu ya Yesu. Mungu amehakikisha kwamba haya mafundisho yamehifadhiwa ili yatufikie sisi na tuyasome kwa Biblia. Wakristo wa kwanza walisoma vitabu vya Agano la Kale pekee, lakini mitume waliendelea kuandika. Mitume waliandika Agano Jipy. Kwa hivyo Mungu ametupa sisi Biblia yote yenye inatwambia kila kitu chenye tunahitaji kujua juu Yake, mipango yake na kusudi lake na juu ya Yesu. Biblia ndiyo kitabu cha kipekee kinachotwambia haya yote.

Tunahitajika kujikaza kusoma Biblia. Kusoma Biblia ni jambo tunalotakiwa tufanye kila siku kwa maisha yetu. Ni vyema kama unaweza kujaribu na uwe na mpangilio, uchague ni wakati gani utakufaa ili usome Biblia kila siku. Ni vyema kufuata mpangilio huo wa kusoma ili usome Biblia yote.

Paulo alishauri kijana msaidizi wake Timotheo ‘aendelee na mwenendo aliojifunza’ kwa sababu ‘Injili inafaa kuhekimisha ili apate wokovu katika Yesu Kristo.’

## **Ushirika**

Inaweza kuwa ni vigumu kuendelea kuwa kwa kitu kama ungali uko kwa mambo yako binafsi. Itakuwa ni vigumu kama utabaki bila ushauri kutoka kwa watu wengine. Mungu anaewela tunachohitaji na himizo kutoka kwa wenzetu. Mungu anataka tuwe kwa ushirika na wenzetu. Ushirika ni urafiki kwa sababu tunainuana na Mungu ametaka hivyo kwa sababu ni muhimu. Ina baraka lakini lazima tuwe na bidii.

Ushirika ni tofauti na urafiki au uanachama wa klabu penye wanachama wana mahitaji sawa. Tofauti ni kwamba tunakuwa na ushirika na Mungu na Yesu na ni muhimu sana. Baada ya ubatizo tunakuwa wana au binti wa Mungu na ndugu au dada wa Yesu Kristo. Uhusiano wetu na Mungu ni wa maana sana. Vivyo hivyo kama ilivyo kwa familia, kila mtoto huwa na uhusiano na baba yake na hii inawafunganya pamoja.

Katika familia ya kiroho, uhusiano wetu na Mungu, ni kama ule na baba zetu. Huu ni ushirika na Mungu na Yesu. Waumini wengine ni watoto wa Mungu pia, kwa hivyo tunawaita ndugu na dada. Tunakuwa na ushirika nao pia. Huu ushirika ni wa kipekee na ni zaidi ya urafiki na kanisa inakuwa familia yetu. Mtume Yohana anaieleza namna hii, "Tunawambia chenye tumeona na tumesikia, ili muwe na ushirika na sisi: na ushirika wetu uko na Baba, na Mwanawe, Yesu Kristo."

Sababu ni ya maana sana kuwa na ushirika na Mungu, kwa hivyo inatubidi tuwe na ushirika wa kweli na watu wenye wana imani moja Kwake. Kwa hivyo haitakuwa vyema kwenda kwa kanisa ya huduma yenye hawaamini Ukweli unaofundishwa kutoka kwa Neno la Mungu yaani Biblia.

Kama kwa familia zetu, si rahisi kuwa marafiki na ndugu au dada wote kwa kanisa. Tunapenda watu wengine kuliko wengine. Lakini kama familia zetu za kawaida, tunatakiwa tujifunze kukaa pamoja. Yesu alitwambia kwamba lazima tujali ndugu na dada. Tukipitana au tugombane, lazima tusulushe haraka badala ya kuwacha mpaka iwe jambo kubwa.

Mungu ametuwekea ushirika ili itusaidie tuwe karibu naye. Kwa hivyo tunahitajika kuweka ushirika wa kuwa pamoja na ndugu na dada kama jambo la maana. Kukiwa na uchaguzi kwamba tunaenda kanisani au kufanya shuguli zingine, lazima uchague kwenda kanisani.

## **Kumega mkate**

Kumega mkate ni sherehe ndogo ya kukumbuka kwamba Yesu alitoa uhai wake na akafa kwa ajili yetu.

Yesu alikula chakula cha jioni cha mwisho na wanafunzi wake. Mwishowe alichukua mkate akaumega na akapeana maombi ya shukurani kwa Mungu. Alipea wanafunzi huo mkate na kila mmoja akachukuwa kidogo na kula. Yesu aliambia wanafunzi, "Huu ni mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Halafu Yesu alitwaa kikombe cha divai na akaambia wanafunzi, "Hiki kikombe ni agano mpya kwa damu yangu imwagiayo kwa ajili yenu; fanyeni hivi kila mnywapo kwa ukumbusho wangu." Baadaye Yesu na wanafunzi waliimba wimbo. Huu ulikuwa mkutano wa kwanza kumega mkate.

Mkutano wa kumega mkate ni wa kukumbuka maisha na kifo cha Yesu. Ni kukumbuka tumaini kuu la uzima tulionayo kwa sababu Yesu alitoa uhai wake kwa ajili yetu. Mkutano huu hautakiwi kuwa na madoido mengi. Sio lazima uwe na watu wengi. Haijalishi kama mko kwa jengo au la. Kama kuna watu wawili au zaidi ya Wakristo wamekutana kwa kukumbuka Yesu, Yesu mwenyewe atakuwa pale nao. Hili ni tulizo kuu, lakini lazima kuwe na heshima na utaratibu na ukweli.

Wanafunzi walikuwa wakikutana mara kwa mara wa kimega mkate. Kawaida ilikuwa mara moja kwa siku ya kwanza ya juma (Jumapili). Walichagua siku hii kwa sababu ndiyo yenye Yesu alifufuka tena ilikuwa siku kuu na hapo wanafunzi walikuwa na nafasi ya kukutana kwa urahisi. Wakristo huwa wanakutana Jumapili kwa sababu Jumapili sio siku ya kwenda kazini. Ingawaje siku haijalishi – cha maana ni kukutana mara kwa mara wakitii amri ya Yesu kumkumbuka. Waliobatiswa pekee yao ndio wanamega mkate na kunywa divai kwa sababu wana ushirika na Mungu na wao wenyewe kwa wenyewe.

## **Maombi**

Maombi ni kuzungumza na Mungu. Kuna faida kuu kuzungumza na Mungu aliyeumba ulimwengu. Tunazungumza naye kama Baba wetu.

Tunafurahi tukizungumza na jamii na marafiki kila wakati. Tukizungumza na marafiki ndio inasaidia uhusiano wetu kukua. Vivyo hivyo na Mungu, tunatakiwa tuzungumze naye mara kwa mara. Tukiomba hivyo tunapata usaizizi na faraja. Yesu alizungumza na Mungu kupitia kwa maombi mara nyngi. Watu wengi wanapenda kuomba asubuhi, jioni na wakati wa chakula. Danieli aliomba mara 3 kwa siku.

Jifunze na uchague kuishi kama Mkristo kwa maisha yako yote. Lakini fuata mwenendo wa Wakristo wa kwanza na ujitee kwa Mungu wewe mwenyewe na utakuwa karibu na Mungu kila siku.